

Zama ni mkubwa!

 Michael Oguttu

 Vusi Malindi


 Matteo E. Mwita

 Kiswahili


 Level 2

(imageless edition)






Mdogo wangu anachelewa
kuamka. Mimi naamka mapema
kwa sababu mimi ni mkubwa!



Mimi ndiye ninayeruhusu jua
kuingia ndani.




“Wewe ni nyota wangu wa
asubuhi,” anasema mama.




Naoga mwenyewe, sihitaji msaada.




Naweza kustahimili maji ya baridi
na sabuni ya bluu inayonuka.




Mama ananikumbusha, “Usisahau
kupiga mswaki.” Namjibu,
“Kamwe, sio mimi!”




Baada ya kuoga, nawasalimu babu
na shangazi, na kuwatakia siku
njema.




Najivisha nguo mwenyewe. “Mimi
ni mkubwa sasa mama,”
ninamwambia.




Ninaweza kufunga vishikizo na kurekebisha viatu vyangu.



Na ninahakikisha mdogo wangu
anapata taarifa zote za shule.



Darasani najitahidi sana katika kila kitu.



Ninafanya hivi vitu vyote vizuri kila siku. Ila kitu ninachokipenda sana ni kucheza na kucheza.



Storybooks Canada

storybookscanada.ca

Zama ni mkubwa!

Written by: Michael Oguttu

Illustrated by: Vusi Malindi

Translated by: Matteo E. Mwita

This story originates from the African Storybook (africanstorybook.org) and is brought to you by Storybooks Canada in an effort to provide children's stories in Canada's many languages.



This work is licensed under a Creative Commons
[Attribution 3.0 International License](http://creativecommons.org/licenses/by/3.0/).